



**SHERIA YA MAREKEBISHO YA KUMI NA MOJA YA KATIBA YA
ZANZIBAR YA 1984**

MPANGILIO WA VIFUNGU

VIFUNGU

MAELEZO

**SEHEMU YAKWANZA
UTANGULIZI**

1. Jina fupi na Kuanza Kutumika.
2. Kusomwa.

**SEHEMU YAPILI
MAREKEBISHO YA VIFUNGU MBALI MBALI**

3. Marekebisho ya Kifungu cha 66.
3. Marekebisho ya Kifungu cha 79.



SHERIA NAM 8 YA 2016

NIMESAINI

{DR. ALI MOHAMED SHEIN}

RAIS WA ZANZIBAR NAMWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

19th October, 2016

SHERIA YA MAREKEBISHO YA KUMI NA MOJA YA KATIBA YA ZANZIBAR YA 1984.

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Kumi na Moja ya Katiba ya Zanzibar ya 2016 na itaanza kutumika kuanzia tarehe 6 Aprili, 2016.

Kusomwa.

2. Sheria hii itasomwa pamoja na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambapo katika Sheria hii itajulikana kama “Katiba”

SEHEMU YA PILI MAREKEBISHO YA VIFUNGU MBALI MBALI

Marekebisho ya Kifungu cha 66.


3. Kifungu cha 66 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno “vyenye uwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi” yaliyopo baina ya maneno “Vyama vya Siasa” na “iwapo hakuna Kiongozi wa Upinzani”

Marekebisho ya Kifungu cha 79

4. Kifungu cha 79 (2) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno “kifungu cha 62 (3)” yaliyopo baina ya maneno “Bila ya kujali masharti ya” na “cha “Katiba” na kuweka badala yake maneno “kifungu cha 78 (4)”



Umepitishwa na Baraza la Wawakilishi, tarehe 29 Septemba, 2016.


RAYA ISSA MSELLEM }
KATIBU, BARAZALA WAWAKILISHI
ZANZIBAR